

OFISI YA RAIS

BODI YA MISHAHARA NA MASILAHU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**HOTUBA YA MGENI RASMI, KATIBU MKUU OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA ALIYOITOA KATIKA
UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA TIMU YA UKUSANYAJI TAARIFA ZA
TATHMINI YA KAZI KWENYE UKUMBI WA JENGO LA MAENDELEO
YA JAMII TAREHE 25 JANUARI, 2016**

**Ndugu, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto,**

**Ndugu, Katibu Mtendaji, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika
Utumishi wa Umma,**

Ndugu, Makatibu Wasaidizi,

Ndugu, Wakurugenzi,

Ndugu, Wakurugenzi Wasaidizi,

Ndugu, Wataalam kutoka Deloitte Consulting Ltd,

Ndugu, Washiriki wa Mafunzo,

Mabibi na Mabwana,

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuyawezesha yote haya yaliyoko mbele yetu leo. Aidha, ninamshukuru Katibu Mtendaji wa Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma kwa maelezo yake mazuri sana ya utangulizi na kwa

kunikaribisha katika kufungua mafunzo haya ambayo ni ya muhimu sana kwa mustakabali wa masilahi ya watumishi wa umma. Mimi binafsi nafurahi kupata fursa hii ya pekee kushiriki katika mchakato wa kuboresha mishahara katika Utumishi wa Umma katika hatua hii ya awali kabisa. Ninapenda vile vile kumpongeza M/S Deloitte Consulting Ltd, Mtaalam Mwelekezi, kwa kupewa jukumu la kuendesha mafunzo haya na hatimae zoezi la Tathmini ya Kazi.

Ndugu washiriki, kama mnavyofahamu, kazi inayofanyika leo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2010 ambayo imetokana na juhudi za Serikali za muda mrefu katika kuboresha mishahara na masilahi ya watumishi wa umma. Nashukuru kuona tunaendelea kushughulikia mambo yaliyoelekezwa katika Sera hiyo.

Ndugu Washiriki, Sote tunafahamu kwamba lengo la kuanzishwa kwa Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ni kuhakikisha kuwa Mishahara na Masilahi mengine yanawianishwa na kuoanishwa ili kuweza kuwavutia na kuwabakiza wataalam katika Utumishi wa Umma. Zoezi la Tathmini ya Kazi sio zoezi jipya katika utumishi wa umma. Zoezi la aina hii lilifanyika mwaka 1998 – 2000 ingawa halikuhusisha utumishi wa umma wote. Zoezi la sasa litapima uzito wa kazi katika utumishi wote wa umma kama ulivyoainishwa katika Hati maalum iliyoanzisha Bodi. Hivyo, kazi iliyo mbele yenu ni kubwa na inahitaji umakini wa hali ya juu. Nimefahamishwa kuwa kundi hili linajumuisha watumishi wa umma wenye weledi katika taaluma mbalimbali na mnaotoka katika maeneo ya pembe zote za nchi yetu.

Ndugu washiriki, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba kazi hii itawahusu watumishi wa umma wote, ni dhahiri kwamba mtakutana na watu wa kada, taaluma, uelewa na matarajio tofauti ambapo mtalazimika kutumia weledi wenu wa mahusiano na mawasiliano (interpersonal and communication skills) katika kufanikisha kazi hii kwa ufasaha.

Ndugu Washiriki, ni matumaini yangu kwamba mtakuwa wasikivu na wepesi wa kuelewa mafunzo haya kwani lengo letu si kuwapa ujuzi wa kufanya kazi hii peke yake bali kuwajengea uwezo katika kumudu mazoezi kama haya kwa siku za baadae. Naelewa kuwa baadhi yenu mlishiriki katika zoezi la mwaka 1998 – 2000 na hivyo natarajia mtatoa mchango mkubwa katika zoezi hili. Nimwombe Mtalaam Mwelekezi kufuatilia kwa karibu utendaji wa kila mshiriki ili kuhakikisha kwamba ameelewa, ameshiriki kikamilifu na kuwa anaweza kuaminiwa siku za baadae kuwa sehemu ya kazi kubwa kama hii. Nitafurahi endapo miongoni mwenu mtatokea wataalam wa kuendesha zoezi kubwa kama hili siku za usoni kama wataalam waelekezi (Consultants).

Ndugu Washiriki, nikamilishe hotuba yangu kwa kuwakumbusha kwamba mafunzo haya na kazi hii ni sehemu ya kazi ya utumishi wa umma, hivyo ninatarajia mtazingatia maadili ya utumishi wa umma katika hatua zote.

Baada ya kusema maneno haya, ninawatakia mafunzo mema na
NINATAMKA KUWA MAFUNZO HAYA YAMEFUNGULIWA RASMI.

ASANTENI SANA